**Maswali na Majibu**

1. Nini iliharibu uhusiano kati ya Adamu na Hawa na Mungu?
   *Adamu na Hawa walifanya dhambi na hii ikaharibu uhusiano.*
2. Mungu ana mpango gani na dunia?
   *Kujaza dunia na watu wazuri.*
3. Nini inatakiwa kabla ya kupata msamaha wa dhambi?
   *Kifo na kumwaga damu.*
4. Waisraeli walipofanya dhambi, walipata msamaha namna gani?
   *Walileta mnyama mkamilifu. Waliweka mkono kwa kichwa yake na kuichinja kama dhabihu.*
5. Huyu mnyama alikuwa analinga kwa nani huko mbele?
   *Alilinga kwa Yesu. Dhabihu ya Mungu iliyokamili.*
6. Mbona kifo cha Yesu msalabani kilikuwa dhabihu iliyokamilifu?
   *Kwa sababu Yesu aliishi maisha kamilifu. Hakutenda dhambi.*
7. Tunatakiwa tufanye nini ili dhambi zetu zisamehewe?
   *Tutubu dhambi zetu, tuwe na imani kwa Yesu, tubatizwe na tukiri dhambi zetu.*
8. Nani aliharibu ukuta uliokuwa katikati yetu na Mungu? *Yesu.*
9. Tunatakiwa tuwe watu wa aina gani?
   *Watu walio na tabia za Mungu – huruma, tukusa, vumilivu, wazuri na kweli.*
10. Toleo la Yesu kama dhabihu imetufanyia nini?
    *Imesaidia kusamehewa dhambi zetu. Imetusaidia kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Imetupa tumaini ya uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu hapa duniani.*

## Mistari ya kukariri

Zaburi 51:1 – 2 Waebrania 9:28 1 Yohana 2:1 – 2

## Mazungumzo

Zungumza vile Yesu kama dhabihu inatupa tumaini la uzima wa milele kwa Ufalme wa Mungu. soma Warumi 12:1. Ni vipi tunaweza kuwa dhabihu iliyo hai?

## Kuandika

Mbona dhambi inatutenga sisi na Mungu. Dhambi zilisamehewa namna gani wakati wa Agano la Kale? Tunatakiwa tufanye nini ili tusamehewe dhambi zetu?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 38 Wokovu katika Yesu

**SOMA Mwanzo 3; Zaburi 51:1 – 2; Walawi 17:11; Warumi 3:23 – 25; Warumi 6:3 – 4; Waebrania 9:22 na 26 – 28; 1 Yohana 2:1 – 2; Mathayo 26:26 – 28**


**SOMO**

Yesu alikuwa mtu mnyofu. Hakufanya dhambi. Mbona alikufa? Kifo chake kinatuletea tumaini la wokovu namna gani? Kila mtu katika maisha yake anaadhiriwa na dhambi. Mungu alisema kila mtu atendaye dhambi lazima afe. Kwa hivyo tunaweza kuwa na tumaini la wokovu namna gani?

Hapo mwanzo Adamu na Hawa waliishi kwa bustani ya ajabu ya Edeni. Walikuwa na uhusiano wa karibu sana na Mungu. Lakini waliasi amri ya Mungu. Walitenda dhambi. Baada ya kutenda dhambi, huo uhusiano na Mungu uliharibika. Hukumu yao ilikuwa kifo. Asili ya miili yao ilibadiliswa ili iteswe kwa magonjwa, na iwe na kuzeeka. Pia walifukuzwa kutoka kwa bustani ya Edeni na kuwa mbali na Mungu.

Dhambi ya Adamu na Hawa iliharibu uhusiano wakaribu na Mungu. Jambo mbaya sana na adhabu kwao ilikuwa watengane na Mungu. Dhambi ilikuwa kama ukuta mrefu katikati yao na Mungu.

Kutoka wakati wa Adamu na Hawa, watu wote wamefanya dhambi. Dhambi za watu zimeharibu mpango wa Mungu wa kujaza ulimwengu na watu wanaojua utukufu wake na kuonyesha hali yake katika maisha yao. Dhambi inatuzuia kuwa karibu na Mungu. Dhambi ni kama ukuta mrefu kati yetu na Mungu. Wenye dhambi hawawezi kuishi milele kwa Ufalme wa Mungu. Mpango wa Mungu ni kujaza nchi na watu wazuri.



Tukifanya dhambi tunaonyesha kwamba hatufai kuishi milele. Mungu hapendi dhambi na watenda dhambi hawawezi kuishi milele. Mungu hapendi dhambi lakini hawachukii wenye dhambi. Lakini dhambi inatutenga na Mungu.

Kwa huruma zake Mungu amewapa watu njia inayoweza kuwaondoa kwa matokeo ya dhambi na kuwaleta karibu naye. Tunatakiwa tuondolewe dhambi na kuoshwa kabisa. Tukiendea Mungu, lazima dhambi zetu zifunikwe. Adamu na Hawa walijaribu kufunika dhambi na uchi wao kwa kujifunika kwa majani ya mtini; lakini hiyo haikukubaliwa na Mungu. Mungu aliwapa nguo kutoka kwa ngozi ya mnyama. Mnyama alichinjwa ndio ngozi ikapatikana. Lazima damu imwagwe ili dhambi ifunikwe.



Biblia inatwambia kwamba inabidi kuwe na dhabihu ya kifo na kumwaga damu ili kuwe na msamaha wa dhambi. Hii inatuonyesha vile dhambi ni mbaya sana mbele ya Mungu. Mungu anahitaji uhai uondolewe kama dhabihu kwa msamaha wa dhambi. Tukifanya dhambi tunatakiwa tufe. Katika Agano la Kale, Mungu kwa huruma zake, aliruhusu mnyama asiye na hatia afe badala ya mtu aliyetenda dhambi.

Sheria za Musa zilliamrisha Waisraeli watoe dhabihu ya mnyama aliyemkamilifu kutoka kwa kundi la mifugo yao. Walipofanya dhambi, walileta mnyama mkamilifu kwa kuhani ndani ya Maskani. Aliyekosa aliweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama kuonyesha uhusiano wa dhambi yake na mnyama atakayetolewa kama dhabihu. Chini ya Sheria hii, Waisraeli walifundishwa kwamba damu ya dhabihu ilimwagwa ili Mungu awasamehe dhambi.

Lakini kifo cha mnyama hakikuleta msamaha wa dhambi milele. Kulikuwa na haja ya dhabihu iliyokamilifu zaidi. Dhabihu ya Agano la Kale haikuwa ya msamaha wa kudumu. Hizi dhabihu zilikuwa zikilenga Yesu ndiye dhabihu kamilifu ya Mungu. Yesu alisema, " Mimi ndimi Njia, Ukweli na Uzima. Hakuna mtu ajaye kwa Baba ila kwa njia yangu."

Yesu alipeana uhai wake kama huduma kwa Mungu. Yesu alijaribiwa kama sisi na angefanya dhambi. Kwa maisha yake yote, Yesu alimenyana na majaribio. Kila wakati alitii mapenzi ya Mungu. Kwa maisha yake yote Yesu alishinda dhambi. Aliishi maisha makamilifu. Kwa sababu aliishi maisha yasiyo na dhambi, kifo chake msalabani kilikuwa dhabihu kamilifu.

Kwa rehema za Mungu, tumepewa wakati wakukubali Yesu kama dhabihu ya dhambi zetu. Kwanza tukubali kwamba tunahitaji wokovu kutoka kwa dhambi na tuwe na imani kwa Yesu Mwokozi. Lazima tutubu dhambi zetu na tuwe na imani kwa Yesu na tubatizwe. Katika ubatizo, dhambi zetu zinaoshwa. Baada ya ubatizo, tunaanza maisha mapya katika Kristo. Bado tutafanya dhambi, lakini tunaweza kusamehewe kila mara, bora tu, tuombe msamaha katika sala zetu. Lazima tufanye bidii tusifanye dhambi, na tukifanya tuombe msamaha katika dhabihu ya Yesu.

Yesu alipeana uhai wake ili sisi tusamehewe dhambi. Yesu ameharibu ukuta wa dhambi. Kupitia kwa Yesu dhambi zetu zinasamehewa na tunakuwa na uhusiano ulio wa karibu na Mungu halafu tunaishi maisha yanayompendeza.




Katika Yesu, dhambi zetu zinafunikwa. Mungu anazifuta na hawezi kuzikumbuka tena. Mungu anapanga kujaza dunia na watu wanaonyesha tabia yake katika maisha yao. Lazima tuulize Mungu atusaidie nasi tujaribu kuwa na huruma, tuvumilie wenzetu na kuwa na ukweli kwa hali yetu. Mungu atatusamehe dhambi zetu katika Yesu. Yesu atakaporudi atafanya yote yaliyomazuri na kweli ndani yetu ili tuishi hapa duniani kwa Ufalme wa Mungu milele.

Baada ya kubatizwa, lazima tukutane kila juma tukila mkate na kunywa divai. Hii inatukumbusha dhabihu ya Yesu. Wakati huu tunakumbuka chakula cha mwisho chenye Yesu alikula na wanafunzi wake. Tunakumbuka vile Yesu alijitoa kama dhabihu, kufa msalabani. Alipeana uhai wake usiokuwa na mawaa kama dhabihu ili dhambi zetu zisamehewe. Tunakuwa na uhusiano wa karibu na Mungu dhambi zetu zikisamehewa. Tunaweza kuwa na tumaini ya ufufuo na maisha ya milele kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani.